



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA  
MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI  
S.L.P. 38 KYAKA - KAGERA

Kumb.Na.KGR/MSY/C.4/7/VOL.III/39

29/03/2021

## **TANGAZO LA KAZI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi alipokea kibali cha Ajira Mbadala, kibali chenye **Kumb. FA.170/368/01'B'/53** cha tarehe **08 Februari, 2021** kwa ajili ya kuajiri Watendaji wa **Kijiji III** nafasi (2)

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Missenyi anakaribisha maombi ya kazi kutoka kwa watanzania wenyе sifa na uwezo wa kujaza nafasi wazi za kazi 2 kwa kada iliyoinishwa hapa chini.

### **MTENDAJI WA KIJIZI (VILLAGE EXECUTIVE ) DARAJA III NAFASI 2**

#### **1.1 MAJUKUMU YA KAZI**

- i. Mtendaji na mshauri wa Halmashauri ya Kijiji na Kamati zake katika mipango ya maendeleo ya kijamii na utekelezaji wa mpango ya maendeleo.
- ii. Kusimamia ulinzi na Usalama wa Raia na mali zao, kuwa mlizi wa amani na msimamizi wa utawala bora katika Kijiji.
- iii. Afisa masuhuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji na atakayesimamia mapato na matumizi ya Halmashauri ya Kijiji.
- iv. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya Kijiji.
- v. Katibu wa Kamti ya Halmashauri ya Kijiji.
- vi. Kutafsiri Sera, Utaratibu na kusimamia utekelezaji wa sheria ndogongogo za Halmashauri katika Kijiji.
- vii. Kusimamia na kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.

- viii. Kuongoza vikao vya maendeleo ya kijiji vitakavyohusisha wananchi na wataalam waliopo kwenye eneo lake.
- ix. Kuhamasisha wananchi katika mikakati mbalimbali ya kuondoa njaa.
- x. Kusimamia matumizi bora ya nguvu kazi.
- xi. Kuratibu na kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika kijiji chake na kuziwasilisha kwenye Kata.
- xii. Kutekeleza shughuli nyingine atakazopangiwa na mwajiri.

## **1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

Kuajiriwa mwenye Elimu ya kidato cha nne au sita aliyehitimu mafunzo ya astashahada /cheti NTA LEVEL 5 katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, usimamizi wa fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo-Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali,

## **1.3 MSHAHARA**

Kwa kuzingatia ngazi za mishahara ya Serikali TGS B


### **MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE WA KAZI**

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania mwenye umri usiozidi miaka 45.
- ii. Mwombaji aambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anwani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
- iii. Mwombaji aambatishe cheti cha kuzaliwa.
- iv. Barua ya maombi iandikwe kwa mkono.
- v. Maombi yote yaambatane na cheti cha taaluma, maelezo, na nakala za vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingaia sifa za kazi husika.
  - Certificates.
  - Cheti cha mtihani wa kidato cha IV na VI
  - Computer Certificate
  - Vyeti vya kitaaluma (Professional Certificates from respective board)
  - Picha moja "Passport size" ya hivi karibuni.
- vi. Testimonials "provisional results" results slips ", kiapo cha kuthibitisha umri wa kuzaliwa **HAVITAKUBALIWA**.
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).

- viii. Waombaji wa Nafasi za Ajira waliostaafishwa/ kuacha kazi katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Katibu Mkuu kiongozi.
- ix. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliw ahatua za kisheria.
- x. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelezo yaliyo katika Waraka Na.  
**CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010.**
- xi. Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe **20/04/2021** saa 9:30 alasiri.
- xii. Maombi yatakaowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili hayatifikiriwa.
- xiii. Maombi yote yatumwe kwa njia ya posta kupitia anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi ~~M~~ Mtendaji wa Wilaya,  
Halmashauri ya Wilaya ya Misserenyi,  
S.L.P 38,  
**KYAKA- MISSENYI.**

**LIMETOLEA NA:**



Innocent M. Mukandala

**MKURUGENIZ MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MISSENYI**